



KARIBU UWEKEZE  
KATIKA HALMASHAURI  
YA WILAYA YA MLELE

Tunatekeleza

www.mleledc.go.tz



HALMASHAURI YA WILAYA

**MLELE**

TAREHE 5 FEBRUARI 2021

**ZIARA YA MJUMBE WA HALMASHAURI KUU YA TAIFA NA MLEZI WA MKOA WA KATAVI MHE, PEREIRA SIRIMA ALIYOIFANYA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE**



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mlezi wa Mkoa wa Katavi Mhe, Pereira Sirima akikagua daraja la Koga lililoko Wilaya ya Mlele baada ya kukamilika ujenzi wake uliogharimu kiasi cha shilingi 4.4 bilioni ambalo ni kiungo muhimu kwa kuunganisha Mkoa wa Katavi na Tabora. wengine ni wajumbe wa kamati ya Siasa ya Mkoa wa Katavi na Wilaya ya Mlele wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Katavi Beda Katani kulia kwake ni Meneja wa Wakala wa barabara nchini Mkoa wa Katavi Martin Mwakabende.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mlezi wa Mkoa wa Katavi Mhe, Pereira Sirima akitoa maelekezo kwa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa na Wilaya baada ya kukagua miradi ya maendeleo katika wilaya ya Mlele, ikiwa ni maazimisho ya miaka 44 ya kuanzishwa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM)

**CCM 5.2. 2021 MIAKA 44**



Mwonekano wa Daraja la Koga baada ya kukamilika ujenzi, Daraja hili linaunganisha Mkoa wa Katavi na Tabora.

*Imeandaliwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mlele*



Meneja wa Mkoa wa Katavi wa Tanroad Martin Mwakabende akitoa maelezo kuhusu ujenzi wa daraja la koga kwa Mlezi wa CCM Mkoa wa Katavi Mhe.Pereira Sirima alipotembelea na kukagua barabara inayojengwa kwa kiwango cha lami akiambatana na kamati ya Siasa Mkoa,pia alikagua maendeleo ya ujenzi wa daraja la Koga lililojengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 4.4 na limekamilika kwa asilimia 98.



Wananchi wa Halmashauri ya Mlele wameungana na wajumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa na Wilaya katika ziara ya mjumbe wa Halmashauri kuu ya Taifa na Mlezi wa CCM Mkoa wa Katavi kukagua miradi ya maendeleo katika kuadhimisha miaka 44 ya CCM katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.

**KARIBU UWEKEZE KATIKA HALMASHAURI YA  
WILAYA YA MLELE. PAMOJA TUNATEKELEZA 2021**



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele Mhe. Soud Mbogo kushoto na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mlele Alexius R. Kagunze wakiwa katika kikao cha Baraza la Madiwani kujadili mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2021/22.



**ILANI YA CCM KWA AJILI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020**

**UMOJA NI USHINDI**



Mchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele Alfred Sungura akitoa taarifa ya Maendeleo ya ujenzi wa mradi wa Jengo la Utawala kwa Mjumbe wa NEC Taifa na Mlezi wa CCM Mkoa wa Katavi Mhe, Pereira hayupo pichani kushoto kwa mchumi ni Afisa Utumshi wa Wilaya Samson Medda ambaye ni Kaim Mkurugenzi na Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari Mr Timothy.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mlezi wa Mkoa wa Katavi Mhe, Pereira Sirima katikati akikagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, kushoto kwake ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa Mhe Beda Katani na mbele ni Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Mlele Mhe, O. Pinda pamoja na mkandarasi wa ujenzi SUMA JKT.



Jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Mlele linaloendelea kujengwa moja ya mradi uliotembelewa na Kamati ya siasa Mkoa na wilaya wakati wa ziara ya Mlezi wa Mkoa wa Katavi Mjumbe wa Halmashauri kuu ya Taifa Mhe, Pereira Sirima hayupo pichani.

***Imeandaliwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mlele***